**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO KIKUU CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI MUHIMBILI

**OFISI YA NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO - TAALUMA**

---

## MAHAFALI YA KUMI NA TISA YA MUHAS

Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) Prof. David Mwakyusa atawatunukia diploma na digrii mbalimbali wahitimu wa MUHAS, katika Mahafali ya Kumi na Tisa yatakayofanyika Alhamis tarehe **04 Desemba 2025** kuanzia saa **tatu asubuhi** katika Kampasi ya Muhimbili.

Wahitimu wote waliofaulu mitihani yao MUHAS na wanastahili kutunukiwa diploma na digrii mbalimbali na wamepanga kuhudhuria mahafali wanakumbushwa:

a) Kulipia TZS 42,000 kama gharama ya kukodisha joho la mahafali kwa kuingia kwenye tovuti ya MUHAS (www.muhas.ac.tz) ili uweze kupata muongozo wa jinsi ya kulipia.

b) Kufika Chuoni kwa ajili ya kuchukua joho la mahafali siku ya **Jumatatu tarehe 17 Novemba** hadi **Jumatatu tarehe 01 Desemba 2025**. Majoho yatachukuliwa kwenye ofisi za Skuli na Taasisi husika kuanzia **saa 4 asubuhi mpaka saa 10 jioni**.

c) Kufika Chuoni kwa ajili ya mazoezi na Wakuu wao wa Skuli na Taasisi siku ya **Jumatano tarehe 03 Desemba 2024 saa 2:30 Asubuhi** bila kukosa (**wahitimu wote ambao hawatahudhuria mazoezi haya hawataruhusiwa kushiriki kwenye mahafali**). Wageni waalikwa, wahitimu pamoja na ndugu na marafiki wa wahitimu wanaombwa wawe wameketi kwenye nafasi zao ifikapo **saa 3:30 asubuhi** siku ya **Ahamis 04 Desemba 2025**

Sherehe za Mahafali zitatanguliwa na sherehe za kuwapa zawadi wanafunzi waliofanya vizuri kitaaluma kwa mwaka **2024/2025** (*Prize Giving Ceremony*) siku ya **Jumatano tarehe 03 Desemba 2025 saa 8:00 mchana**.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi - Muhimbili S. L. P. 65001, DAR ES SALAAM

Prof. Emmanuel Balandya

**NAIBU MAKAMU MKUU WA CHUO – TAALUMA**

9 Barabara ya Umoja wa Mataifa, Upanga Magharibi; S.L.P 65001, Dar Es Salaam: Simu: +255-22 2151596/2150302-6; Ext: 1236; Nukushi:+255-22-2150465; Barua pepe:dvcarc@muhas.ac.tz;Tovuti: https://www.muhas.ac.tz